

FORM 1 TERM 3 APRIL 2022

KISWAHILI

SEHEMU YA A: INSHA ALAMA 20

Andika insha itakayoanza kwa:

Tuliamka asubuhi ya majogoo tayari kwa safari tulioingojea kwa siku nyingi...

SEHEMU YA B : UFAHAMU B ALAMA 20

Mavazi Rekebisheni

Vazi jema kivaliwa, huongeza heshima,
Staha mtu kapewa, pote endapo daima,
Mavazi duni si sawa, kina dada ninasema,
Mavazi rekebisheni, usherati umezidi.

Longi kwa nyuma kushika, na mapajani kubana,
Chupi zilipowafika, dhahiri kuonekana,
Bure munaabikia,na kujishusha maana,
Mavazi rekebisheni, usherati umezidi.

Kifuani kujikaza, maziwa yaning'inie,
Kitu gani munawaza, hamna habari nyie,
Ni ashiki mwasambaza, sikizeni niwambie,
Mavazi rekebisheni, usherati umezidi.

Msichana ni hatia, magotini kufichuka,
Hivyo basi kuvalia,rinda lisoyafunika,
Huenda zusha hisia, maovu yakawafika,
Mavazi rekebisheni, usherati umezidi.

Kuwa wazi kinenani, hupendeza Baniani,
Kwao mila ya zamani, si kujitakia shani,
Weusi twatafutani, kuiga za Ulayani,
Mavazi rekebisheni, usherati umezidi.

Sitakosa kuzitaja, skati mnazovaa,
Zaisha kwa mapaja,kikiri kuchuchumaa,
Iko wazi nyonga moja, mkato ulivyokaa,
Mavazi rekebisheni, usherati umezidi.

Wazi nitawosomea, nguo hizi nguo gani ?
Dada zetu mwakosea, kuzivaa hadharani,
Ndizo hizo huchochea, usherati mitaani,

Mavazi rekebiseni, usherati umezidi.

Nguo chini zishusheni, mwilini mzipanue,
Heri kuingia deni, za heshima mnunue,
Kuigiza za kigeni, ni utumwa mtambue
Mavazi rekebiseni, usherati umezidi.

Beti tisa namaliza, kalamu naweka chini,
Iwapo wajiuiza, nakereketwa ni nini ?
Ni staha nahimiza, sio wake kuhaini,
Mavazi rekebiseni, usherati umezidi.

- a) Shairi hili ni la aina gani? (alama 1)

.....

- b) Shairi hili lina beti ngapi? (alama 1)

.....

- c) Eleza vina vya ubeti wa kwanza . (alama 1)

.....

- d) Shairi hili lina kibwagizo au kimalizio? Kwa nini ? (alama 1)

.....

- e) Taja tatu nne za mavazi ambazo msanii ana kashifu. (alama 3)

.....

.....

- f) Kwa kuzingatia maudhui ya shairi hili , fafanua methali : (alama 2)
Chema chajuza, kibaya chajitembeza.

.....

.....

.....

- g) Eleza umbo la shairi. (alama 4)

.....

.....

.....

h) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (alama 3)

i) staha-----

ii) ashiki-----

iii) twatafutani-----

MATUMIZI YA LUGHA C: (alama 35)

a) Toa tatu mbili za irabu i (al3)

b) Taja sauti mbili ambazo ni vipasuo vya ufizi (al2)

c) Eleza maana ya silabi kwa kutolea mfano (al2)

d) Maneno yafuatayo yana silabi ngapi? (Al2)

- i. Maktaba -----
ii. Mwanafunzi -----

e) Unda neno moja lenye sauti mwambatano (al1)

.....

f) Andika sentensi zifuatazo bila ya kutumia kirejeshi amba--- (al2)

Fulana ambayo imefumwa ni nyekundu

.....
.....

g) Tunga sentensi mbili kudhihirisha tofauti kati ya: (al4)

- i. Tata.....
ii. Dada.....

h) Taja vipashio vine vya lugha. (al4)

.....
.....
.....
.....

i) Andika sentensi hii katika ukubwa wingi (al2)

Mtu mrefu alianguka pu!

-
.....
.....
- j) Bainisha maneno katika sentensi ifuatayo. (al3)
Mzazi ataenda mjini.
.....
.....
.....
- k) Ainisha viambishi katika sentensi. (al2)
Nilikimbia
.....
.....
.....
- l) Toa matumizi mawili ya mkwaju (/). (al2)
.....
.....
.....
- m) Weka maneno yafuatayo katika ngeli zao. (al 3)
i. Mbuyu.....
ii. Kifaru.....
iii. Chai.....
- n) Sahihisha sentensi ifuatazo. (al1)
Huko ndimo alimopatikana.
.....
.....
.....
- o) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika wakati ujao. (al1)
Mimi ninapenda mtoto mtiifu
.....
- p) Andika wingi wa: (al2)
Mtoto ataenda shulen.
.....
- q) Kanusha (al1)
Nitaruka kamba.
.....
- r) Pang'a maneno haya ili kupata sentensi sahihi
Mbegu mkulima nyingi amepanda. (al 2)
.....
.....

SEHEMU D:ISIMUJAMII. [ALAMA 10]

- a) Eleza maana ya sajili ya lugha. [alama 2]
.....
.....
- b) Taja mambo manne yanayosababisha kuibuka kwa sajili tofauti. [alama 4]
.....
.....
.....
.....
- c) Huko ukitoa mifano eleza sifa nne za sajili ya sokoni. (alama 4)
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

SEHEMU YA E: FASIHI ALAMA 15

- a) Fafanua aina mbili za fasihi (alama 2)
.....
.....
- b) Eleza sifa nne za mtambaji bora (alama 4)
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

c) Eleza aina mbili za ngano

(alama 2)

d) Taja sifa tatu za fasihi simulizi

(alama 4)

e) Fafanua aina tatu ya wahusika katika fasihi simulizi.

(alama 3)
